TANGAZO LA SERIKALI NA. 432 la terehe 11/7/2025

SHERIA YA BARABARA,
(SURA YA 167)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(1))*

KANUNI ZA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAEGESHO KATIKA HIFADHI ZA BARABARA ZA KITAIFA ZA MWAKA 2025

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Fasili.

SEHEMU YA PILI
UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA MAEGESHO

4. Uanzishwaji wa maegesho.
5. Majukumu ya mamlaka ya barabara.
6. Majukumu ya Bodi.
7. Wajibu wa mmiliki wa chombo cha moto.

SEHEMU YA TATU
UENDESHAJI WA MAEGESHO

8. Uwekaji na matumizi ya mfumo wa kielektroniki.
9. Viwango vya ada ya maegesho.
10. Mtoa huduma.
11. Muda wa kutoza ada ya maegesho.
12. Msamaha wa kulipa ada ya maegesho kwa baadhi ya vyombo vya moto.

13. Maegesho maalum.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

14. Upotevu au uharibifu wa chombo cha moto au mali.
15. Kinga dhidi ya madai.
16. Makosa na adhabu

SHERIA YA BARABARA,
(SURA YA 167)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(1))*

KANUNI ZA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAEGESHO KATIKA
HIFADHI ZA BARABARA ZA KITAIFA ZA MWAKA 2025

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Usimamizi na Uendeshaji wa Maegesho katika Hifadhi za Barabara za Kitaifa za Mwaka 2025.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika barabara zote za kitaifa.

Fasili

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada ya maegesho" maana yake ni malipo ya kutumia maegesho;

"barabara za kitaifa" maana yake ni barabara kuu na barabara za mikoa kama zilivyoainishwa katika kifungu cha 12(2) cha Sheria;

Sura ya 220

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Mfuko wa Barabara iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta;

"chombo cha moto" maana yake ni chombo kinachoendeshwa barabarani kwa kutumia mfumo ulio ndani yake kwa dhumuni la usafirishaji wa mtu, watu au mizigo;

"hifadhi ya barabara" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"maegesho" maana yake ni eneo lililotengwa ndani ya hifadhi ya barabara kwa ajili ya kuegesha chombo cha moto;

"maegesho maalum" maana yake ni maegesho ndani ya hifadhi ya barabara yaliyojengwa na kuainishwa na mamlaka ya barabara kwa lengo la kuegesha vyombo vingi vya moto kwa wakati mmoja;

TS. Na. 293 la 2000

"mamlaka ya barabara" maana yake ni Wakala wa Barabara Tanzania ulioanzishwa kwa Amri ya Uanzishwaji wa Wakala wa Barabara Tanzania;

"mmiliki wa chombo cha moto" maana yake ni mmiliki halali wa chombo cha moto na inajumuisha, mtumiaji aliyeruhusiwa au mtu aliyehifadhi chombo cha moto kwenye maegesho;

"mtoa huduma" maana yake ni mtu au taasisi iliyoteuliwa na Bodi kusimamia utekelezaji wa Kanuni hizi; na

Sura ya 167

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Barabara.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA MAEGESHO

Uanzishwaji wa maegesho

4. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria na Kanuni hizi, mamlaka ya barabara inaweza kuainisha, kujenga, kufanya matengenezo na kuruhusu matumizi katika eneo lililotengwa ndani ya hifadhi ya barabara kwa ajili ya maegesho.

Majukumu ya mamlaka ya barabara

5. Bila kuathiri ujumla wa kanuni ya 4, mamlaka ya barabara itakuwa na majukumu ya-

(a) kuweka alama au kiashiria cha kuzuia au kuruhusu kuegeshwa kwa chombo cha moto

au aina ya chombo cha moto kwenye maegesho;

(b) kuweka alama katika eneo la maegesho zinazoonesha makadirio ya upana au urefu wa chombo cha moto kinachoruhusiwa kuegeshwa katika maegesho;

(c) kuzuia kwa kufunga chombo cha moto kwenye maegesho kwa kushindwa kulipa ada na adhabu, au kuegesha vibaya;

(d) kuondoa, na ikibidi, kuhifadhi mali yoyote itakayokutwa kwenye eneo la maegesho kinyume na utaratibu uliotolewa katika Kanuni hizi;

(e) kuuza kwa mnada wa hadhara mali yoyote ambayo itakuwa imehifadhiwa kwa kipindi kinachozidi siku tisini kwa amri ya mahakama; na

(f) kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa utekelezaji wa Kanuni hizi.

Majukumu ya Bodi

6. Kwa madhumuni ya kuwezesha usimamizi na uendeshaji wa maegesho ulioainishwa katika Kanuni hizi, Bodi itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kumshauri Waziri juu ya viwango vipya vya ada ya maegesho kwa kuzingatia hadhi ya eneo husika, aina ya chombo cha moto na muda uliotumika na chombo hicho kwenye maegesho;

(b) kuweka viwango vya ada ya maegesho vitakavyotumika kwa maegesho na maegesho maalum;

(c) kugharamia ujenzi, matengenezo na usalama wa maegesho;

(d) kuingia na kusimamia mikataba ya huduma au hati za makubaliano kwa ajili ya utekelezaji wa Kanuni hizi;

(e) kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa utekelezaji wa Kanuni hizi; na

(f) kutoa miongozo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa maegesho.

Wajibu wa mmiliki wa chombo cha moto

7.-(1) Mmiliki wa chombo cha moto anayetumia eneo lolote la maegesho lililo chini ya usimamizi wa Kanuni hizi atawajibika kulipa ada ya maegesho kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni hizi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

(2) Endapo mmiliki wa chombo cha moto atashindwa kulipa ada ya maegesho kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kutolewa kwa ankara, atawajibika kulipa ada anayodaiwa pamoja na faini isiyopungua asilimia ishirini ya ada anayodaiwa.

(3) Mmiliki wa chombo cha moto atakayeshindwa kulipa ada ya maegesho pamoja na faini kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani, atawajibika kwa adhabu ya jumla iliyoainishwa kwenye Sheria.

## SEHEMU YA TATU
## UENDESHAJI WA MAEGESHO

Uwekaji na matumizi ya mfumo wa kielektroniki

8. Bodi itaweka mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya-

(a) kuchukua picha ya kibao cha namba ya usajili ya chombo cha moto kilichoegeshwa katika maegesho kwa ajili ya utambuzi wa taarifa za chombo husika;
(b) utoaji wa ankara ya ada ya maegesho na taarifa nyingine muhimu kwa mmiliki;
(c) ulipaji wa ada ya maegesho kupitia mfumo wa malipo ya kielektroniki;
(d) kutoa stakabadhi ya malipo ya ada ya maegesho;
(e) kutambua chombo cha moto kinachodaiwa ada ya maegesho; na
(f) upokeaji wa taarifa au malalamiko kutoka kwa wamiliki wa vyombo vya moto.

Viwango vya ada ya maegesho

9.-(1) Viwango vya ada ya maegesho vitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

(2) Bodi inaweza kupendekeza kwa Waziri kuhusu marekebisho ya viwango vya ada ya maegesho kadiri itakavyoona inafaa.

Mtoa huduma

10.-(1) Bodi inaweza kuingia mkataba na mtu, kikundi cha watu au kampuni kama mtoa huduma kwa madhumuni ya kusimamia na kuendesha maegesho.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, mtoa huduma atawajibika kutoza na kukusanya ada ya maegesho kutoka kwa mmiliki wa chombo cha moto anayetumia maegesho kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mfanyakazi wa mtoa huduma, atatakiwa kuwa na kitambulisho cha kazi na kuvaa sare maalum ikiwa na nembo ya Bodi na ya mtoa huduma muda wote akiwa anatekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

Muda wa kutoza ada ya maegesho

11.-(1) Mmiliki wa chombo cha moto atatozwa ada ya maegesho katika muda wowote atakapoegesha chombo chake katika maegesho kwa zaidi ya dakika tano.

(2) Mtu au taasisi inaweza kulipia maegesho yaliyokaribu na makazi ya watu au taasisi kwa matumizi ya shughuli maalum kwa muda usiozidi siku moja.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni hii, ada ya maegesho itatozwa kwa saa, siku, wiki, mwezi au mwaka kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Msamaha wa kulipa ada ya maegesho kwa baadhi ya vyombo vya moto

12.-(1) Vyombo vya moto vifuatavyo havitatozwa ada ya maegesho ya chombo cha moto:

(a) chombo cha moto kinachomilikiwa na Serikali ambacho kina namba ya usajili inayotumika kwa vyombo vya moto vya Serikali;

(b) chombo cha moto kinachomilikiwa na taasisi yenye hadhi ya kidiplomasia ambacho kina namba rasmi ya usajili inayotumiwa na taasisi hiyo;

(c) chombo cha moto kilichoegeshwa katika maegesho yaliyo jirani na eneo linalotumika kwa muda huo kwa shughuli za kitaifa;

(d) chombo cha moto kinachotumika kusafirishia wagonjwa; na

(e) chombo cha moto kilichoegeshwa katika maegesho yaliyo jirani na eneo la maziko ambako kuna tukio la mazishi kwa wakati huo.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Bodi inaweza, kwa sababu za msingi, kutoa kibali kwa mtu yeyote au taasisi ili kutumia maegesho bila kulipa ada ya maegesho.

Maegesho maalum

13.-(1) Mamlaka ya barabara inaweza kuendeleza eneo kubwa la maegesho ndani ya hifadhi ya barabara kwa lengo la kuwezesha vyombo vingi vya moto kuegeshwa kwa wakati mmoja.

(2) Pamoja na mambo mengine, maegesho maalum yatakuwa na malango ya kuingilia na kutokea vyombo vya moto pamoja na huduma muhimu za kijamii.

(3) Bodi itakuwa na wajibu wa kugharamia uendelezaji na uendeshaji wa maegesho maalum.

(4) Viwango vya ada ya maegesho kwenye maegesho maalum vitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Upotevu au uharibifu wa chombo cha moto au mali

14. Bodi, Mamlaka ya Barabara au mtoa huduma hatahusika na upotevu au uharibifu utakaotokea kwa chombo cha moto au mali itakayokuwa ndani ya chombo cha moto wakati kikiwa kwenye maegesho.

Kinga dhidi ya madai

15. Bodi, mamlaka ya barabara au mtoa huduma hatawajibika kwa kosa la madai kutokana na kufanya au kutokufanya jambo lolote kwa nia njema katika kutekeleza masharti ya Kanuni hizi.

Makosa na adhabu

16.-(1) Mtu yeyote au mmiliki wa chombo cha moto ambaye-

(a) atafanya biashara yoyote kwenye maegesho bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mamlaka ya barabara;
(b) ataweka kizuizi kwenye maegesho;
(c) ataegesha kimakosa; au
(d) ataegesha chombo cha moto cha aina, ukubwa au uzito uliokatazwa kwenye maegesho,

anatenda kosa na iwapo atatiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa kwenye Sheria.

(2) Mtu au mmiliki wa chombo cha moto atakayeharibu au kusababisha uharibifu wa miundombinu ya maegesho, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa kwenye Sheria pamoja na kulipa fidia sawa na gharama ya matengenezo ya miundombinu hiyo kulingana na tathmini itakayofanywa na mamlaka ya barabara.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni za 9(1) na 13(4))*

(a) Ada za Maegesho katika Barabara za Kitaifa

| Hadhi ya Eneo | Aina ya Chombo cha Usafiri | Ada ya Maegesho kwa Saa (TZS) | Ada ya Maegesho kwa Siku (TZS) | Ada ya Maegesho kwa Wiki (TZS) | Ada ya Maegesho kwa Mwezi (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam | Pikipiki yenye magurudumu mawili | - | 300 | 1,500 | 6,000 |
| | Pikipiki yenye magurudumu matatu | - | 500 | 2,500 | 10,000 |
| | Gari | 500 | 2,500 | 12,500 | 50,000 |
| | | | | | |
| Halmashauri ya Jiji la Arusha na Mwanza | Pikipiki yenye magurudumu mawili | - | 300 | 1,500 | 6,000 |
| | Pikipiki yenye magurudumu matatu | - | 500 | 2,500 | 10,000 |
| | Gari | 500 | 1,500 | 7,500 | 30,000 |
| | | | | | |
| Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Mbeya, Tanga na Manispaa zote | Pikipiki yenye magurudumu mawili | - | 300 | 1,500 | 6,000 |
| | Pikipiki yenye magurudumu matatu | - | 500 | 2,500 | 10,000 |
| | Gari | 300 | 1,000 | 5,000 | 20,000 |
| | | | | | |
| Halmashauri za Miji | Pikipiki yenye magurudumu mawili | - | 200 | 1,000 | 4,000 |
| | Pikipiki yenye magurudumu matatu | - | 300 | 1,500 | 6,000 |
| | Gari | - | 500 | 2,500 | 10,000 |
| | | | | | |

(b) Viwango vya Ada ya Maegesho Maalum

| | Aina ya Chombo cha Usafirishaji | Ada ya Maegesho kwa Saa [TZS] | Ada ya Maegesho kwa Siku [TZS] |
|---|---|---|---|
| 1 | Gari ndogo | 500 | 4,000 |
| 2 | Gari inayozidi tani 1.5 lakini haizidi tani 3 | 1,000 | 8,000 |
| 3 | Gari inayozidi tani 3 lakini haizidi tani 10 | 1,500 | 10,000 |
| 4 | Gari inayozidi tani 10 | 2,000 | 15,000 |

Dodoma,
25 Juni, 2025

ABDALLAH HAMIS ULEGA
*Waziri wa Ujenzi*